Madam Deputy Speaker, I will be more comfortable because the two days have been my days. I want to be very sincere in whatever I say without guessing.

First and foremost, I thank the 30 or so Senators who have voted. Some of them are even---

The Deputy Speaker (Sen. (Prof.) Kamar): That is just the exception because you were busy in the last two days. Otherwise, when you start you---

Sen. Kibiru: Yes, Madam Deputy Speaker. You start and finish in the same language.

Thank you, Madam Deputy Speaker. As I was saying, I take this opportunity to thank the 12 or so Senators who participated in the debate of the Budget Policy Statement (BPS), and more so, the Senators who have spent time and voted for the Motion.

Just like most the Senators have said, this is one of the most crucial debates or legislation that the Senate needs to pass.

As I conclude, I ask that when we go out there, lobbying must be done. Sen. Olekina, Justice Madzayo and others we need to lobby that the Government listens to us, that we need Kshs485 billion. Sen. Wetangula, we want to send you to tell the principals wherever you meet them that the Senate for once would want Kshs485 billion to go to counties. Let us not have a debate when we come to the Dollar. It is something that we have made a resolve and I pray that when time comes, we will all stand up and defend our last chance to ensure that funds get to the devolved entities.

Madam Deputy Speaker, having said that, I wish my fellow Senators, the Secretariat and those who have been working with us more so the people of Kirinyaga County and my fellow Kenyans, a Merry Christmas and a very rewarding 2022. I would also say that come next year - like somebody has wished us - next December, I think I will be the Governor of Kirinyaga County. I thank you.

(Laughter)

The Deputy Speaker. (Sen.(Prof.) Kamar): Proceed, Sen. (Dr.) Musuruve

Sen. (Dr.) Musuruve: Asante sana Bi Naibu Spika kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Hoja hii. Nawashukuru maseneta wenzangu kwa kazi tuliyo fanya mwaka huu. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tumeweza kuunda sheria ingawa pia kuna zingine ambazo hazijakamilika.

Ni jukumu letu kuendelea kuunda sheria bila kuchoka. Ninajua kwamba wakati tutarejea vikao vya Seneti mwaka kesho, tutajikakamua kuja hapa na kuzungumzia mambo ya sheria kwa sababu waKenya wanatusubiri na wanataka kuona tunawatetea. Seneti inajukumu la kutetea wakenya na hiyo ndiyo kazi yetu. Nawaahidi walemavu kwamba sitachoka; nitaendelea kuwatetea hapa Seneti. Ninashukuru Seneta wenzangu kwa sababu nikizungumzia maslaha ya walemavu huwa wanajiunga nami na tunaweza kuhakikisha walemavu wamepata haki yao.

Tutaendelea kuzungumza kuhusu sheria ya lugha ya ishara. Nataka kuwahakikishia walemavu katika nchi yetu ya kuwa nina imani Maseneta wenzangu watajiunga nami na watahakikisha kwamba sheria ya lugha ya ishara imepita kikamilifu na pia kupelekwa katika Bunge la Kitaifa. Ni ombi langu kuwa Mswada huo utakapo fikishwa katika Bunge la Kitaifa, hautachelewa na Rais ataweza kuweka muhuri uwe sheria rasmi.

Najua kuwa walemavu wamekuwa na changamoto kwa sababu kuna mambo mengi sana ambayo hayajawekwa kisheria. Sen. (Dr.) Mwaura, pia aliwasilisha Mswada mwingine unaolenga walemavu unajadiliwa na tunaomba kuwa utakuwa sheria kamilifu ili walemavu wapate haki yao.

Disclaimer: The electronic version of the Senate Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor, Senate.

Bi. Naibu Spika, wakenya lazima wajue kwamba tunaenda likizo lakini tutaendelea kuwa viongozi. Tukiwa likizo, nawaomba Maseneta wazidi kuwasiliana na wakaazi wa kaunti zao. Maswala ambayo hayendelei vizuri mashinani, tuyalete hapa Seneti ili wakenya waishi kwa amani.

Ningependa kuwakumbusha wakenya kwamba ingawa tunaenda likizo wanafaa kuwa waangalifu. Huu ugonjwa wa COVID-19 si wa kuchukulia kiholela; ugonjwa huu unaambukiza kina mama, baba na kila mtu. Wakenya wanafaa kuwa waangalifu kwa kuvalia barakoa na kunawa mikono ili ugonjwa huu usiendeleo kusambaa. Tunafaa kuchunga maisha ya wenzetu.

[The Deputy Speaker (Sen. (Prof.) Kamar left the Chair]

[The Speaker (Hon. Lusaka) in the Chair]

Nachukua fursa hii kukushukuru kwa kuwa tumeweza kuwa na mazungumzo mazuri mwaka huu hapa Seneti. Naishukuru Seneti kwa kuhakikisha kwamba ombi zinazoletwa na wakenya zinawekwa katika mstari wa mbele ya kuwa kila Mkenya anapata haki yake. Nawatakia Wakenya wote krismasi njema na mwaka mpya wenye mafanikio. Asante.

The Speaker. (Hon. Lusaka): Sen. Wetangula Proceed.

Sen Wetangula: Bw. Spika, asante sana kwa kunipa fursa hii kuchangia yale wenzangu wamesema tunapofikia kikomo cha muhula huu wa mwaka huu. Kwanza ni kukushukuru wewe Bwana Spika na kikundi chako, wakiwemo Naibu Spika, Sen. (Prof) Margaret Kamar na wale wenzetu waliomo kwa jopo la Spika na ambao mara kwa mara huchukua nafasi ya kukaa katika kiti chako na kuongoza mijadala ya Seneti hii kwa njia ya heshima na ambayo inastahili sifa.

Mwaka huu wote hatujawai kuwa na taharuki yoyote katika Bunge hili; hata wakati ambao tulikuwa tumeganyika kuhusu ugavi wa pesa, ilifanyika kwa njia ya heshima. Kila mtu alitoa maoni yake, ikasikizwa, ikakubalika na ikaheshimimka. Bunge la Seneti limejitenga kama Bunge la kuaminika. Kama ndungu yetu anayewakilisha Kaunti ya Kilifi amsema, Bunge la Seneti lina Maseneta wenye vipaji mbali; tuna maprofesa, mawakili, madaktari na pia mahandisi. Maseneta walioko hapa wanatajriba mbali mbali.

Tunapotamatisa vikao vya Seneti vya mwaka huu, tuangazia kule tumetoka, tulipo na tunako elekea na kujivunia kuwa tumepitisha Miswada na Hoja nyingi ambazo zinaleta mabadiliko kwa Wakenya.

Jana tulijadiliana kuhusu *Budget Policy Statement* (BPS) au Sera ya bajeti na kauli kutoka hazina kuu ambayo inahusu bajeti ijayo. Maseneta walichangia hoja hiyo kwa uwazi na wakasema kuwa hata liwe liwalo, eneo za ugatuzi zinahitaji kuongezewa pesa kwani huko ndiko wananchi wa Kenya wanaishi na hivyo wanahitaji kupewa huduma zinazotakikana kwa mfano, matibabu, elimu za chekechea na vitu vingine.

Nikimalizia, nawaomba wenzangu katika uwanja wa kisiasa wawe wakarimu wanapoendeleza kampeni. Wakenya wengi watuona sisi wanasiasa kana kwamba tumegeuza uwanja huo kuwa uwanja wa fujo. Nataka kuomba sote tukubaliane

kuwa hata tukibishana kutafuta viti vya uongozi, mwisho wa mabishano lazima tulinde amani ya nchi yetu. Tuhakikishe ya kwamba akina mama, watoto, walemavu na wale ambao kwa njia moja au nyingine hawajiwezi au ni wanyonge, wawe na nafasi ya kulindwa na sisi sote.

Bw. Spika, mwaka huu umekuwa na changamoto haswa kwangu na wewe pia kwa sababu tunatoka kaunti moja. Unajua kuwa tulimpoteza Mbunge wetu wa Kabuchai. Nashukuru Maseneta ambao walituma pole zao. Tulimzika na kwenda kwa uchaguzi mdogo ambapo tulimchagua mrithi wake na sasa tunaendelea vizuri.

Kibinafsi pia nilimpoteza ndugu yangu mdogo kwa huu ugonjwa wa Korona. Kwa hivyo, tukizungumzia Korona, mjue kwamba wengine wetu tumefikiwa na ugonjwa huu. Nilimpoteza mama ndogo na nawashukuru sana nyote mliotuma rambirambi zenu.

Bw. Spika, Mungu yuko na Mungu hubaki Mungu, hana jina lingine. Wale wakorofi waliotaka kuvuruga chama chetu cha FORD-Kenya, walishindwa vibaya. Tukikutana na wale ambao walikuwa wanawaunga mkono, wana haya na hawataki kutusalimia. Wanatoroka wakituona kila mahali tukienda.

Nataka kuwashukuru hawa ndugu zetu wote hapa Seneti ambao kwa njia moja au nyingine walikuwa wakija kwangu pole pole kuniambia: “tuko pamoja na wewe, tunakuombea na hii utashinda.” Na tulishinda!

Bw. Spika, wale ambao wameshindwa tunawaambia tumewasamehe lakini hatutasahau, kwa sababu wamejifanya kuwa vibaraka wa wengine na kwa siasa ya nchi yetu hatutaki vibaraka. Tunataka watu wenye msimamo, heshima na wale wanazingatia demokrasia katika maisha yao kibinafsi, katika vyama vyao na katika nchi yetu.

Bw. Spika, tukielelekea katika uchaguzi mkuu, tunakuunga mkono vile umekuwa ukisema mara kwa mara ya kwamba tunahitaji uchaguzi wenye usawa, haki, ukweli na amani. Hii ni kwa sababu nchi yetu imepitia changamoto kubwa ya mabishano ya uchaguzi mwaka wa 2007 mpaka tukapoteza maisha na mali ya Wakenya.

Bw. Spika, tukiangalia nyuma, ile funzo tumesoma ni kujua ya kwamba katika mabishano ya kisiasa, uchaguzi ukiisha tunabaki kuwa Wakenya na lazima tuendeleo kufurahia na kujivunia kuwa Wakenya.

Kwa polisi wetu, tunaenda kwa hafla za Krisimasi. Tunawaomba mfanye kazi kusaidia wananchi ili tusiwe na misongamano isiyo na maana katika barabara zetu. Tupunguze ajali ili Wakenya wanaotoka hapa jijini kwenda mashinani, iwe ni Pwani, kaskazini au magharibi na popote pale, waweze kusafiri bila kuhangaishwa na majambazi barabarani au bila kurundikana na milolongo ya magari kwa sababu ya kutoajibika kwa polisi wanaolinda trafiki kwa barabara.

Bw. Spika, nachukua nafasi hii kuwatakiya Wakenya na kuwapatia salamu za heri na fanaka katika mwezi huu wa Krisimasi. Tunajua wamekuwa na changamoto nyingi. Wakenya wengine watasherehekea Krisimasi bila chakula, wengine wanaenda wakihangaika kutafuta karo za watoto kwa sababu shule zinafunguliwa mwezi ujao.

Tunaomba Wizara ya Elimu iwachilie pesa za basari ziende kwa shule na kwa wale wanaohusika ili katika wiki mbili au tatu zijazo, shule zikifunguliwa, watoto waweze kwenda shule wakijua hayo ndiyo maisha yao ya baadaye.

Bw. Spika, tunamshukuru Rais wetu na kumpatia heri ya Krisimasi. Tunampatia pia Naibu Rais heri ya Krisimasi na haswa wenzangu katika uongozi wa One Kenya

Alliance (OKA); ndugu zangu, Mhe. Kalonzo Musyoka, Mhe. Musalia Mudavadi, Sen. Gideon Moi, Mhe. Cyrus Jirongo na wale wote ambao wamesema wataungana na sisi. Tunawaomba tuchangie vilivyo kama Wakenya wengine tukijua uchaguzi unakuja na lazima uwe wa haki, usawa, ukweli na wa amani.

Bw. Spika, Mungu atubariki sisi sote. Turudi mwezi ujao kama Maseneta tukijua ya kwamba leo tumepigania kuongeza pesa kwa kaunti zetu. Tuwe na huo msimamo, kwa sababu kama uchumi umekuwa, lazima kaunti pia zipate mapato yanayokua.

Asante, Bw. Spika.

The Speaker (Hon. Lusaka): Sen. (Prof.) Kamar.

Sen. (Prof.) Kamar: Thank you, Mr. Speaker, Sir, for giving me the opportunity to join my colleagues in wishing ourselves a very Merry Christmas.

The Speaker (Hon. Lusaka): What is your point of order, Sen. Wetangula?

Sen. (Prof.) Kamar, take your seat.

Sen. Wetangula: Mr. Speaker, Sir, is it in order for the distinguished Senator for Uasin Gishu County, who ordered that this afternoon all our well wishes and farewell for the year must be in Swahili--- She must understand and know that what is good for the goose must be good for the gander.

The Speaker (Hon. Lusaka): Basi Profesa umejikaanga na mafuta yako. Jiokoe sasa.

(Laughter)

Sen. (Prof.) Kamar: Mr. Speaker, Sir, I started presiding in English and now I do not want to break the rules of the Speaker. I was stuck with that one.

(Laughter)

The Speaker (Hon. Lusaka): Hoja ya nidhamu ni gani, Sen. Madzayo?

Sen. Madzayo: Asante, Bw. Spika. Tulipokua hapa leo mchana, kumetolewa amri na naibu wako. Sio *Emeritus* Sen. Wako. Nasema naibu wako wewe, Naibu wa Spika wa Bunge la Seneti.

Akasema leo, kwa vyovyote vile, liwalo liwe, Maseneta wote ambao wako ndani ya Bunge la Seneti kuagana hapa leo, ikiwa ndio tarehe yetu ya mwisho, wataongea Kiswahili. Je, ni haki? Hata huyu mdogo wangu, ndugu yangu ninayemuenzi sana, Sen. M. Kajwang' ana Kizungu mufti, lakini leo ameona aongee lugha ya mama.

Bw. Spika, nataka nikuulize wewe kwa kauli moja, je, ni haki kwa Naibu wako, ambaye tunamuenzi sana hapa ndani ya Bunge letu, kuvunja amri yake mwenyewe aliyoweka hapa na kila mtu ameifuata?

The Speaker (Hon. Lusaka): Naagiza kwamba Naibu wa Spika atumie lugha ya Kiswahili.

(Laughter)

Sen. (Prof.) Kamar: Asante sana, Bw. Spika. Ningependa kuungana na Maseneta wote kukushukuru kwanza kwa kazi nzuri huu mwaka wa 2021.

(Laughter)

Bw. Spika, nashangaa kwa nini Sen. Olekina aliye shindwa kabisa kuongea Kiswahili anacheka. Leo ni siku ya maana sana kwa sababu tumeamua tutaongea Kiswahili kusema asante.

Shukrani ya kwanza ni kwako Bw. Spika. Shukrani ya pili ni kwa *Panel* yako na tumefanya kazi nzuri. Shukrani ya tatu ni kwa sisi sote Maseneta. Tumefanya kazi nzuri sana mwaka huu wa 2021.

Bw. Spika, leo ilikua siku nzuri sana kwa sababu tulivunja rekodi. Kwa kura, tulikuwa na Maseneta 30 kwenye mtandao na ndani ya Bunge. Ningependa kuwashukuru sana kwa sababu walituheshimu. Tuliitisha Kikao hiki kiwe Kikao Maalum, na tukakuja sote. Nina washukuru sana.

Bw. Spika, la mwisho ni kutakia kila mtu heri, fanaka na Krismasi njema, sio tuu kutakia Maseneta, bali pia watu wa Kaunti ya Uasin Gishu, wenye walinileta hapa. Nawatakia Krismasi njema na mwaka mpya wa baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Asante, Bw. Spika.

The Speaker (Hon. Lusaka): Pongezi sana.

Sen. Farhiya: Asante, Bw. Spika, kwa kunipa fursa hii kuchangia mjadala huu. Wacha hata mimi nijaribu leo. Hua napigia Maseneta simu kila siku nikiwaomba wapigie mjadala fulani kura. Nina washukuru sana kwa kuitikia mwito wangu kila wakati.

Nina wahimiza Wakenya wachukue chanjo kama wanataka tupigane na Korona na maisha yetu iendelee vile ilikua inafaa kuwa. Serikali inatoa chanjo bure. Watu waende kwenye hospitali na wapewe chanjo.

Bw. Spika, nina wahimiza magavana walipe watu pesa ambazo wanandaiwa. Walipe watu wa mashinani pesa ili watu waanze kujiokoa kutokana na umaskini ambao umeletwa na ugonjwa wa Korona.

Nina wahimiza Maseneta kuwa Mungu akitujalia tupate fursa ya kukutana hapa tena mwaka ujao, tuta pitisha mijadala mingi. Hii ni kwa sababu tuko karibu kumaliza muhula wa Seneti hii. Tusiwache watu wamefanya bidii wakaleta Miswada hapa Bunge na waende nyumbani bure bilashi bila kupitisha Miswada yao. Ningependa Spika wetu atumie ushawishi wake kuhakikisha kwamba Bunge la Kitaifa lipitishie Miswada yetu ili iwe sheria.

Bw. Spika, tuko na fursa nzuri katika historia ya taifa letu kwa sababu tunatengeneza sheria ya kufanikisha ugatuzi. Sheria hizo ni nzuri na ni lazima zipite ili wananchi wapate mafanikio ya ugatuzi. Nina washukuru Maseneta kwa kutetea ugatuzi wakati wowote kulingana na jukumu lao.

Ninawasihi Wakenya kuwa watu wanao wania kiti cha urais ni wengi sana. Kila mmoja anajirembesha kuwa yeye ndiye mzuri zaidi. Ninawaomba Wakenya waweke watu ratil ili wahakikishe kwamba yule wanampea mamlaka anafaa kuendesha nchi yetu mbele.

Bw. Spika, ninashukuru kila mtu kwa huu mwaka ambao tumemaliza vizuri zaidi. La mwisho ni ningependa kuwatakia Wakenya, Maseneta, sekretarieti na kila mtu ambaye anatusaidia kuendesha shughuliza za Seneti sikukuu njema.

Asante, Bwa. Spika.

The Speaker (Hon. Lusaka): Sen. (Dr.) Milgo.

Sen. (Dr.) Milgo: Asante, Bw. Spika. La kwanza ni kuchukua fursa hii kushukuru viongozi wa Seneti na Maseneta wenzangu jinsi tumeendelea mwaka huu na miaka nne iliyopita.

Ninakumbuka siku ya kwanza ulipotupeleka *orientation*. Ninakumbuka nilikuuliza kama nitawahi weza kutunga sheria hata moja. Leo hii ninaposimama hapa nimepitisha Miswada yangu zaidi ya mbili na Hoja mbali na zile za Kamati, na bado ninaendelea.

Bw. Spika, nina kushukuru kwa njia umetuelekeza na kutufunza. Nimepata kujifunza kutoka kwa Maseneta wenzangu namna ya kuendeleza mambo ya siasa. Hapo awali nilikuwa mwalimu. Sasa hivi nimegeuzwa na kuwa mwanasiasa kamili.

Ningependa pia kushukuru wengazu kwa kupitisha *Budget Policy Statement (BPS)*, ingawa bajeti hiyo haina pesa za kutosha kuenda mashinani. Inamaanisha kwamba huduma kule mashinani hazitatimizwa kikamilifu, haswa tukiangalia upande wa elimu.

Mimi binasfi nimepata kujua kwamba mambo ya wanafunzi kugoma kila wakati ni kwa sababu ya upungufu wa matumizi katika shule na msongamano katika bweni na vyumba vya mamkuli. Ninafikiri kwamba tukiendelea kuongelea haya mambo, Serikali kuu itaongezea pesa ili mambo kama haya yaweze kuangaliwa ili huduma zipeanwe inavyo stahili.

Bw. Spika, msimu huu si wa Krismasi pekee bali pia ni msimu wa siasa. Ningependa kuhimiza Wakenya wenzangu kwamba wakati huu sio wa kuenda kupiga kura mara ya mwisho. Tutapiga kura mwaka wa 2022 na bado tutakuwa na miaka ingine ya kupiga kura. Kwa hivyo, tujitenge na mambo ya kupigana. Lazima tukae tuskize kila mwanasiasa. Kama vile imesemwa, kuna wengi wanawania kiti cha urais. Vile vile kuna wale wawania kiti cha Seneta, Gavana na Wawakilishi Wodi. Tunasahili kukaa na kuskiza hawa kisha tukate kauli bila kupigana. Ni lazima tujue kwamba baada ya ya siasa hawa wakubwa wana salimiana na kunywa chai pamoja. Hatutaki kumwaga damu bila sababu.

Bw. Spika, ningependa kutakia Wakenya wote kila la heri, haswa watu wangu wa Kaunti ya Bomet. Wahakikishe kwamba wakati huu wa Krismasi, wajitenge na mambo ya kuchangamka bila kuhakikisha wamefuata maagizo ya Wizara ya Afya. Mbali ya hayo, wahakikishe kwamba wamepata chanjo ya COVID-19. Hii ni kwa sababu hivi sasa kuna aina ya Korona mpya inaitwa *Omicron* na ni hatari sana. Tayari tuko na chanjo za kutosha katika vituo vya afya na chanjo hazina madhara yoyote.

Bw. Spika, la mwisho, ningependa kutakia kila la heri Maseneta wenzangu, Nawatakia Krismasi njema na mwaka mpya wenye fanaka.

The Speaker (Hon. Lusaka): Sen. (Eng.) Hargura.

Sen. (Eng.) Hargura: Asante, Bw. Spika kwa kunipatia nafasi hii. Langu ni kuungana na wenzangu, Masenta walio hapa Bungeni, kuwashukuru Maseneta wote kwa kazi tuliyo weza kufanya mwaka huu katika kutimiza majukumu yetu kama wawakilishi wa serikali za ugatuzi na watungi wa sheria.

Bw Spika, kama mwakilishi wa Kaunti ya Marsabit katika Seneti, nina huzunika sana katika hali ambayo mwaka huu na miaka mitatu iliyopita imekuwa kwa wakaazi wa

Kaunti ya Marsabit. Kwa bahati mbaya kulikuwa na ukosefu wa amani katika Kaunti ya Marsabit na watu wengi wamepoteza maisha yao takriban zaidi ya watu 100. Kuna wakati hesabu ilikuwa ilifanywa. Mali nyingi imeibiwa na nyumba kuchomwa. Ni huzuni sana kwangu kuwakilisha kaunti kama hii katika Seneti.

Kila wakati tunajaribu kutatua hali hii na kwa bahati mbaya ni vita na ukosefu wa amani ambao unatokana na viongozi na wanasisia ambapo mpaka sasa hali haijatulia na haijabadilika. Inaendelea tu kuharibika. Naomba Mwenyezi Mungu tukiwa tunaelekea wakati wa siasa aweze kutupatia njia ya kutatua shida hii. Ni kwa sababu ni wakati ambao tutakuwa na changamoto nyingi sana kwa sababu ya kuchochea watu.

Bw Spika, ninawahimiza viongozi wote waliochaguliwa katika Kaunti ya Marsabit katika nyanja mbali mbali ikiwa ni kutoka Members of County Assembly (MCAs) mpaka magavana na viongozi wengine wote ambao pia wanahusika katika hali moja ama nyingine katika katika Marsabit, tukae pamoja tuweze kutatua Hali hii. Viongozi wakikosana haimaanishi kwamba mpaka tuhusishe raia kupatikane vifo na mali kuhalibiwa. Kuna njia nyingi sana ya kutatua tofauti za kisiasa.

Nataka kuwashukuru wazee kutoka jamii tofauti za Kaunti ya Marsabit hasa wale 53 ambao walijaribu na bado wanaendelea kuleta amani haswa wale wenyevidi kutoka jamii tofauti wakiongozwa na kijana Jacob Elisha. Wiki mbili zilizopita walikuja Nairobi kwa warsha ya mambo ya amani na wakatutafuta sisi viongozi wakasema ni lazima tuweze kukaa chini.

Bw Spika, hakuna kitu kinaendelea katika mji wa Kitale. Biashara zimefungwa, watu wamehama na hata imefika kiwango amri imetolewa hizi piki piki zote zisimamishwe. Sasa uchukuzi umesimamishwa na hali sio nzuri hata kidogo. Mpaka hata jana jioni najua kuna kijana aliuawa. Ni hali ambayo inahuzunisha sana.

Wakati wazee hawa walikuja tulikaa nao kama viongozi na tukasema wote wahusishwe. Tukasema tukae kama viongozi na katika mkutano huo, lazima Gavana wa Kaunti ya Marsabit na Waziri wa Fedha wahudhurie kwa sababu tunajua umuhimu wao katika mambo ya jamii huko haswa katika ukosefu wa amani. Tulikaa na tukakubaliana kwamba tutashauriana na watu wetu wasimamishwe vita. Leo siku ya Jumatano ingekuwa ni siku tungekuwa na mkutano huo huko Marsabit.

Bw Spika, lakini kwa bahati mbaya na kwa sababu ya watu ambao hawataki amani, Jumamosi iliyopita kulitokea mauaji ya zaidi ya watu 13 na mali ikachukuliwa lakini iliweza kurudishwa. Hiyo sasa imevuruga tena ile hali na mpango tulikuwa nayo.

Ninataka kuwahimiza wakaazi wa Marsabit watulie na viongozi tuje pamoja bado turudi tuweze kushikana na wazee wetu na kuwahimiza watu wetu wasimamishwe vita halafu tuanze taratibu ya kujadili njia ya kuleta amani. Vile ambavyo tumeangalia, hivi ni vita ama ukosefu wa amani ambao unatokana na siasa na ni vitu ambavyo lazima viongozi tukae chini tuweze kutatua. Tumejaribu lakini imeshindikana kwa sababu viongozi wengine hawako tayari kukaa na wenzao na jambo hili linachangia ukosefu wa amani.

Bw Spika, pamoja na hayo, nataka pia nielekeze huu ujumbe kwa serikali kuu kwa sababu ni jukumu lao kudumisha amani na kuchunga maisha na mali ya Wakenya wote bila kujali msimamo wao wa kisiasa, jamii au dini. Lazima serikali ihudumie kila

mtu kwa usawa. Lakini hali ambayo tunaona kama wakaazi wa Marsabit sivyo serikali inatuhudumia. Serikali pia katika hii vita imeonekana ni kama inaegemea upande mmoja.

Jamii fulani ikivamiwa, serikali haina habari lakini wengine wakivamiwa ni tofauti. Juzi ilifika kiwango tuliona mara ya kwanza serikali inakuja na nguvu sana kuhakikisha kwamba jamii fulani ikivamiwa wanafuata wale wengine kurudisha mali yao. Lakini hawa wengine wakati walikuwa wanavamiwa serikali hata ukijaribu kuwaambia wachukue hatua, hawataki kujua. Wana lawama na wajue kwamba serikali ni ya kila mtu na inatajikana ihudumie kila mtu.

Bw Spika, katika hii hali ya ukosefu wa usalama kuendelea katika Marsabit mpaka kufika kiwango hiki, yangu ni kusema kwamba hata wao wanachangia kwa sababu ya kutokuwa na uadilifu na usawa katika utendakazi wao. Hao pia kama serikali kuu waweze kuhudumia Wakenya wote na kuchukua hatua bila kujali ni nani analeta hiyo vurugu.

Hii ni kwa sababu naamini kwamba serikali iko na uwezo juu ya kila raia. Ndio maana sikubaliani na yale matamshi ya mratibu wa usalama katika Bonde la Ufa aliposema kwamba kuna wahalifu sehemu za Laikipia wako na silaha kushinda silaha za serikali. Kwa hivyo, ni jukumu la serikali kutumia nguvu zake kudhibiti amani na kuhakikisha Wakenya wanaishi kwa amani. Yangu ni hayo kwa serikali kuu.

Bw Spika, pia ninawahimiza wenzetu viongozi wakati kama huu wa siasa tuendeshe siasa zetu kwa njia ya nidhamu bila kugonganisha Wakenya. Mara nyingi, Wakenya wanaumia tukiwa tunawaelekeza katika njia mbaya.

Ninakushukuru kwa kunipatia fursa hii na kuomba ya kwamba Mwenyezi Mungu atatuweka salama. Mwaka ujao tukifungua Bunge, tuweze kuwa na nguvu ya kuendelea na kazi zetu. Asante.

The Speaker (Hon. Lusaka): Basi kuna wale wamebaki. Nitawaomba niwape dakika tatu. Sen. Omanga, endelea kwa dakika tatu na ni Kiswahili.

Sen. Omanga: Bw Spika, asante. Ningependa pia kujiunga na wenzangu kuwapongeza kwa kupitisha bajeti. Kama Maseneta, kweli tumeonyesha kwamba tunaweza kupigania Uगतuzi na kusaidia kaunti zetu kwa changamoto wanazozipitia. Mwaka huu umekuwa wa changamoto nyingi sana. Tumeathiriwa na ugonjwa wa Coronavirus (COVID-19). Umekuwa mwaka mgumu sana kwetu sisi kama viongozi na wananchi wetu ambao tunawaongoza.

Watu wengi wamepoteza kazi haswa vijana na akina mama na biashara za watu wengi zimeathiriwa. Tunafunga mwaka na bado nasikia kwamba kama bunge hatujaweza kufanya yanayotosha tuweze kusaidia wananchi wetu kurudi pahali walikuwa kabla ya hii changamoto ya COVID-19. Ningependa tukirudi mwaka ujao Mungu akitujalia inshallah mwezi wa pili, tuone vile tunaweza kufanya kama viongozi kuwasaidia wananchi wetu warudi kazini na tuweze kuboresha uchumi wetu na wafanyibiashara waweze kurudi kufanya biashara zao.

Bw. Spika, mwaka huu, Seneti ilipitisha miswada nyingi hata ingawa kuna zingine nyingi ambazo hazijaweza kushughulikiwa kikamilifu katika Seneti. Miswada zingine pia bado zimekwama katika Bunge la kitaifa. Wengi wetu tunahangaika kwa muda mrefu kutayarisha miswada na hata kukosa usingizi lakini zikifika katika Bunge la Kitaifa, zinakosa kushughulikiwa. Seneti inafaa kujadiliana na Bunge la Kitaifa ili

kuhakikisha kwamba miswada inayotoka hapa Seneti hazitupiliwi mbali zinapofika huko. Mara kwa mara miswada inayotoka hapa Seneti hututpiliwa mbali katika Bunge la Kitaifa.

Bw. Spika, nawatakia Maseneta wote Krismasi njema na vile vile wananchi wote wa Kenya sana sana wakaazi wa Kaunti ya Nairobi.

The Speaker (Hon. Lusaka): Sen. (Prof.) Ongeru, muda ni wako sasa.

Sen. (Prof.) Ongeru: Asante sana Bw. Spika kwa kunipa fursa hii kuchangia Hoja hili. Nawashukuru maseneta wenzangu kwa kupitisha hoja la *Budget Policy Statement* linaloangazia ugavi wa fedha kwa kaunti zetu. Bei za bidha kadha wa kadha zimepanda. Serikali za kaunti zina wakati mgumu wa kufikisha kiwango cha bajeti zao.

Nawashukuru wenzangu kwa kupitisha hoja inayowania kuongeza bujeti kwa serikali zetu za ugatuzi. Nitarajia kwamba wakati Wizara ya Fedha itakapo tangaza bajeti mwaka ujao, watatia maanani pendekezo zilizowasilishwa na maseneta leo bila kutafuta mbinu za kushusha kiwango cha fedha kilichopitishwa na Bunge hili leo. Nina imani kuwa serikali za kaunti hazitapata chini ya Kshs485 bilioni. Waziri wa Fedha atakapo leta makisio ya bajeti, tunatarajia kuona kwamba yote tuliyopendekeza yamewekwa katika bajeti bila tashwishi lolote.

Pili, siasa za uchaguzi mkuu wa mwaka wa 2022 zimeanza na nimeona kwamba wanasisia wengi wana tabia ambayo haiwezi kuleta amani katika nchi hii. Nawasihi wanasisia wenzangu watulie kidogo katika harakati za kisiasa ile tuwe na mikakati za kuleta uwiano na amani. Tusitenganishe watu kwa mambo ambayo hayawezi kutujenga. Matamshi yetu katika kampeni yawe ya kulenga umoja na kujenga bali si kubomoa nchi.

Pia, ningependa huwasihii wabunge na viongozi wote wa nchi wawe na heshima. Kama unaenda kutembea katika eneo la mbunge mwingine, unapaswa kumpa kiongozi wa eneo hilo heshima na sio kueneza siasa za uchochezi. Nawasihi wanasisia wote tuwe wataratibu katika mienendo yetu na njia zetu za kisiasa wakati huu wa sherehe za Krismasi na mwaka mpya.

Bw. Spika, nakushukuru kwa kutupa mwelekeo mzuri mwaka huu. Tumekuwa na vikao kadha wa kadha mwaka huu na hivyo tukaweza kuhitimu mambo mengi. Itakuwa fanaka kubwa mwaka ujao tutakaporejea vikao vya Seneti. Nina imani kuwa tutapitisha miswada na hoja zilizobaki kwa maana zina maana sana kwa watu wetu. Haja yetu ni kuboresha maisha ya wananchi wa Kenya katika kaunti zetu ili wananchi wetu haswa vijana, kina mama, wazee na wachuuzi waweze kukuza na kuboresha biashara zao zaidi ya hali ilivyoko sasa.

Mwisho, ningependa kuwakumbusha wananchi wote kwamba bado tunapambambana na janga la COVID-19. Virusi vya COVID-19 vya Omicron ni hatari. Virusi hivyo vinaenea haraka sana kama moto uliowashwa katika kichaka kilichokauka. Nawasihi wananchi wote wajiatharishe zaidi wanapoungana na wenzao. Ugonjwa huo wa COVID-19 umeleta maafa mengi katika jamii zetu. Nawasihi maseneta wenzangu na wakenya kwa jumla kujikinga na COVID-19 kwa sababu ugonjwa huo utaturudisha nyuma zaidi.

Bw. Spika, nachukua fursa hii kuwatakia watu wote wa Kaunti ya Kisii na wakenya wote kwa jumla krismasi njema na mwaka mpya wenye heri.

The Speaker (Hon. Lusaka): Asante sana Sen. (Prof.) Ongeru. Mwisho, nampa Sen. Kavindu Muthama fursa ya kuzungumza.

Sen. Kavindu Muthama: Bw. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Kwanza kabisa nakupongeza wewe na ofisi yako kwa kazi njema ambayo mumefanya mwaka huu. Umetuongoza vyema katika vikao vya Seneti ambavyo tumekuwa navyo mwaka huu.

Pili, nawashukuru maseneta wenzangu kwa ushirikiano mwema ambao wamenipa tangu nilipojiunga na Seneti. Mimi si mchanga kwa umri lakini mimi ni mchanga katika Bunge la Seneti. Nilipokelewa vyema hapa Seneti nilipojiunga mwezi wa tatu. Tangu nilipojiunga, nimeweza kuwasilisha arifa mbali kuhusu mambo yanayowaathiri watu wa Kaunti ya Machakos. Nina imani kuwa arifa hizo zitapitishwa hivi karibuni na kwamba Kaunti ya Machakos itaweza kuorodheshwa kama mojawapo ya eneo zenye ukavu. Kaunti yangu ya Machakos inaendelea kukumbwa na shida ya ukosefu wa maji. Natarajia kwamba swala hilo litakapowasilishwa hapa Seneti, litapitishwa na vile Bunge la Taifa.

Bw. Spika, nawashukuru maseneta wenzangu kwa kupitisha miswada nyingi sana hii tuliyopitisha leo inayolenga kuongezea serikali zetu za kaunti fedha ili waeze kufanya kazi vizuri. Nina furaha kwamba tumepitisha fedha kiasi cha Kshs485 bilioni iende kaunti zetu ili kufaidi watu wetu. Nawasihii magavana kwamba watakapo pokea pesa hizo, wafanye kazi vilivyo ili wasaidie wananchi wa kaunti zao.

Hizo pesa zikifika, tunaomba magavana waweze kufanya kazi inayofaa kwa ajili ya wananchi.

Ninaomba pia Wizara ya Fedha isipunguze bajeti kama vile tulivyosema. Waipitisha vivyo hivyo.

Bw. Spika, Building Bridges Initiative (BBI) ilikuwa imepropose---

(Technical hitch)

The Speaker (Hon. Lusaka): Tumekupoteza.

Sen. Kavindu Muthama: Bw. Spika, nikimalizia, wakati huu wa Krisimasi madereva wengi huenda kwa mwendo wa kasi. Kwa hivyo, ninawaomba waendeshe wananchi kwa usalama ili tusipoteze maisha.

Ninawatakiwa watu wangu wa Kaunti ya Machakos na Kenya kwa jumla, Krisimasi njema yenye baraka za Mwenyezi mungu na mwaka mpya wenye mafanikio.

Ninaomba Wizara ya Elimu na wahusika wote wafanye kila juhudi ili wazazi wanaporudisha watoto shuleni mwezi wa kwanza, watoto wanaotoka kwa familia ambazo hazijiwezi wapate *bursaries* ili wazazi washughulike na vitabu na *uniforms*. Huu wakati ni mgumu sana kwa sababu ya Covid-19; biashara nyingi haziendi vizuri kama ilivyotakuwa kabla ya Covid-19. Kwa hivyo, tujali masilahi ya watu wetu na tusaaidiane inavyostahili.

Bw. Spika, ninakutakia wewe, Maseneta na wananchi wote Krisimasi njema.

Ninaomba tufanye siasa za amani. Wanaosimama kuchaguliwa kama Rais waelekeze watu vyema. Wananchi pia wachague viongozi ambao watasaidia.

Ninatumi tutarudi wote hapa mwezi wa pili tukiwa salama na tutamaliza mwaka vizuri.

Disclaimer: The electronic version of the Senate Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor, Senate.

Asanteni na Mungu awabariki.

The Speaker (Hon. Lusaka): Sen. (Dr.) Mwaura, nilikuwa nimemaliza.

Ninakupa dakika mbili tu.

Sen. (Dr.) Mwaura: Asante Bw. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuwa wa mwisho kuzungumza. Ninawataka Wakenya wote salamu za heri na fanaka msimu huu wa Krisimasi.

Ninaomba demokrasia iweze kudumu ili kila mtu awe na haki ya kujieleza kwa uhuru. Katika msimu huu wa Krisimasi, tuwe na umoja na tuweze kusaidia wale ambao wana kipato cha chini na hawajafaidika kama wengine. Pia tudumishe undugu ndiposa kila mtu ajihisi kama Mkenya.

Tusiangalie tofauti zetu za kisiasa kama jambo la kututenganisha sisi kwa sababu tutakuwa na mirengo mingi ya kisiasa, upande huu utavutia upande ule mwingine. Lakini fauka ya hayo yote, Kenya nzima inafaa kujiendeleza na kujizatiti kwa manufaa ya kila mwananchi.

Pia, ninawahimiza viongozi kutoa misimamo ambayo ata kama itatofautiana kisiasa lakini isilete pingamizi au tofuati za kuwagawanyisha Wakenya.

Bw. Spika, ninakushukuru kwa uongozi wako katika muhula huu wote wa Bunge la Seneti ambao tumeumaliza. Huu ni muhula wa tano katika awamu hii ya Bunge. Hii inamaanisha tumebakisha miezi michache tumalize Bunge la pili la Seneti.

Ninatumi kwamba Wakenya watapiga msasa kuangazia utendakazi wetu na kutupa nafasi za kuendelea kufanya kazi katika Bunge hili, lile lingine au katika kitengo kingine cha uongozi katika nyanja za kijamii.

Ninakushukuru na tuwe na Krisimasi njema na mwaka mpya wenye mafanikio.

The Speaker (Hon. Lusaka): Nami ninachukuwa nafasi kushukuru Bunge la Seneti kwa jumla kwa ustadi na kwa kusimama kama Bunge moja licha ya mawimbi mbalimbali ambayo yalitokea msimu huu. Tumekuwa na mambo mengi lakini tumekaa pamoja kama Bunge la Seneti.

Ninawashukuru sana kwa Miswada ambayo mmeleta ambayo inakinga ugatuzi na kwa maswala ambayo tumezungumzia.

Ninajivunia kama Spika wenu kwa kuongoza viongozi ambao wamekomaa na kuchangia sana kukua kwa ugatuzi katika Jamuhuri yetu ya Kenya.

Sitasahau kushukuru viongozi ambao tunafanya nao, haswa Viongozi wa Waliowengi na Waliowachache na wote walio katika *Senate Business Committee* (SBC). Ninawashukuru kwa sababu pamoja tumefanya kazi kwa kushirikiana na kuorodhesha maswala ambayo yamekuwa yakizingatia sana mambo ya ugatuzi katika nchi yetu.

Ninashukuru pia *secretariat* wakiongozwa na *clerk* na wote ambao wamehakikisha tumekuwa na vikao bila shida yeyote.

Ninamatumaini kwamba Mungu akitupa uhai, tutakutana tena Februari na kuendelea kufanya kazi yetu.

Kama vile Maseneta wengine wamesema, tuendeleo kuzingatia kanuni za afya kwa mambo ya Covid-19. Haswa tukienda mashinani, lazima tuhakikishe kwamba sisi kama viongozi, tuko kwenye mstari wa mbele kuelimisha watu wetu juu ya ugonjwa wa Covid-19.

Nikimalizia, ninachukua nafasi hii kuwatakia Maseneta wote na Wakenya kwa jumla Krisimasi njema na mwaka mpya 2022 wenye mafaniko. Tusherehekee tukijua kwamba, mwaka ujao, kuna majukumu yatakayohitaji tutumie pesa zetu.

Kwa hivyo, hata kama tutakuwa na Krisimasi na mwaka mpya, tusitumie pesa zote halafu Januari, tuwe na shida halafu tuanze kuitisha harambee ya kutimizi maswala fulani.

Kwa hayo, ninawashukuru na kuwatakia Krisimasi njema na mwaka mpya wenye mafanikio.

ADJOURNMENT

The Speaker (Hon. Lusaka): Hon. Senators, there being no other business, it is now time to adjourn the House. The Senate, therefore, stands adjourned until Tuesday, 8th February, 2022, at 2.30 p.m.

The Senate rose at 4.58 p.m.